

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU KUANZA RASMI MATUMIZI YA MFUMO MPYA WA HISA KIGANJANI

Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) linapenda kuwataarifu wawekezaji na umma kwa ujumla kwamba, kuanzia **tarehe 21 Julai 2026**, litaanza rasmi **awamu ya mpito (Transition Phase)** kuelekea matumizi ya **Mfumo Mpya wa Hisa Kiganjani**.

Katika kipindi hiki cha mpito, wawekezaji wote wanahimizwa kuanza kutumia mfumo mpya na kukamilisha uhamaji wao kwa kufuata utaratibu na maelekezo yatakayotolewa rasmi na DSE na kuendelea na miamala katika mfumo mpya.

Tunapenda pia kuwafahamisha kuwa kuanzia **tarehe 1 Agosti 2026**, **mfumo wa sasa wa Hisa Kiganjani utasitishwa rasmi**, na huduma zote za uwekezaji zitaendelea kutolewa kupitia **Mfumo Mpya wa Hisa Kiganjani** pekee.

Ili kuhakikisha unaendelea kupata huduma za uwekezaji bila usumbufu, tunawasihi wawekezaji wote kukamilisha uhamaji wao ndani ya kipindi cha mpito.

DSE itaendelea kutoa maelekezo na taarifa muhimu kuhusu mchakato huu kupitia tovuti na kurasa zake rasmi za mawasiliano.

Tunawashukuru wawekezaji wetu kwa ushirikiano wao na kwa kuendelea kuiamini DSE katika safari ya kuimarisha huduma za uwekezaji kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Kwa mawasiliano

Phone: +255758675655

Email: onlinetradingssupport@dse.co.tz